Dialogue: Noun /ˈdaɪ.ə.lɒg/- Formal talks between opposing countries, political groups conflicting people.

"Dialogue is the best way to incorporate the citizens in community policing."

Mazungumzo: Mawasiliano rasmi baina ya makundi pinzani.

"Masemazano ni njia nzuri ya kushirikisha raia katika ulinzi wa kijumuia."

Dissatisfied: Adjective /dɪsˈsætɪsfaɪd/- A person or group of people or community who are no longer happy or contented with society's values and or practices.

"The dissatisfied youth need to be reassured of their potential in nation building."

Wasioridhishwa: Hawa ni watu ambao hawana imani katika amali za jamii tena.

"Vijana waliochukizwa na wasioridhishwa wanatakikana kuhakikishiwa uwezo wao katika ujenzi wa taifa."

Disconnected youth: Noun- /,dɪs.kəˈnek.tɪd juːθ/- It is used to describe a group of young people who feel that they are not part of a wider community.

"The disconnected youth are prone to joining extremist groups."

Vijana waliojitenga: Hutumika kuelezea kikundi cha vijana wanaohisi kuwa wao sio sehemu ya jamii pana.

"Vijana waliojitenga wamo katika hatari ya kujiunga na vikundi vyenye misi-mamo mikali."

Dispossession: Noun- /,dɪs.pəˈzefən/- The act of taking property, especially buildings or land, away from someone or a group of people.

“Dispossession is a bad activity that can drive people into conflicts.”

Unyakuzi: Tendo la kuchukua milki hasa mijengo au mashamba kutoka kwa watu wengine.

“Unyakuzi ni kitendo kibaya ambacho kinaweza kuelekeza watu kwenye mizozo.”

Divisive politics: Noun- /diˈvaɪ.sɪv ˈpɒl.ə.tɪks/- It is used to describe politics that cause great and sometimes unfriendly disagreement within a group of people.

“Divisive politics makes some communities feel discriminated.”

Siasa za migawanyiko: Hutumika kuelezea siasa ambazo husababisha mitafaruku miongoni mwa watu.

“Siasa za migawanyiko huwafanya watu wajihisi kama waliotengwa.”

Doctrines: Noun - /ˈdɒk.trɪns/- A religious, ideological or political belief (or system of beliefs) accepted as authoritative by some group or school.

“Religious doctrines attribute to radicalization in some communities.”

Kanuni za kidini: Imani ama mfumo wa imani zinazotawala dini ama kikundi fulani cha watu.

“Huenda baadhi ya kanuni za kidini zinachangia katika uchocheaji wa misi-mamo mikali baina ya makundi ya watu.”

Documentation: Noun /ˌdɒk.jə.menˈteɪ.ʃən/- A process of recording/ putting down information on a piece of paper or in soft copy.

“The documentation of all the people in a region should be up to date.”

Unakili katika maandiko: Kuweka katika maandishi taarifa rasmi.

“Unakili watu katika maandiko lazima uhariwe mara kwa mara.”

Do-no-harm approach: Noun- /duː nəʊ hɑːm əˈpreɪtʃ/- A friendly engagement that is expected to yield positive outcome.

“All the parties must adopt a do-no-harm approach when handling delicate societal matters.”

Mtazamo wa kutodhuru: Mwingiliano wa kirafiki ambao mara nyingi huwa na matokeo mema kwa wanaohusika.

“Washika dau wote wanastahili kukumbatia mtazamo wa kutodhuru wana-poshughulikia masuala nyeti ya kijamii.”

Donors: Noun- /ˈdɒʊ.nəs/- Persons or organizations that give money or goods to an individual or another organization or a country.

“The developed countries are among the donors who are helping Kenya in the fight against extremism.”

Wafadhili: Watu au shirika linalotoa msaada wa pesa au bidhaa kwa mtu binafsi, shirika lengine ama nchi.

“Mataifa yaliyoendelea kiuchumii ni miongoni mwa wafadhili wanaosaidia Kenya katika vita dhidi ya misimamo mikali.”

Drug abuse: Noun- /drʌg əˈbjuːz/- To use drugs for the wrong purpose in a way that is harmful or morally wrong.

“Drug abuse could lead someone to become violent.”

Utumizi mbaya wa mihadarati: Kutumia dawa za kulevya.

“Utumizi wa mihadarati unaweza kumfanya mtu akawa na fujo.”

E

Economic deprivation:- Noun- /iː.kəˈnɒm.ɪk ˌdɛp.rɪˈveɪ.jən/- A situation in which you do not have things or conditions that are usually considered necessary for a pleasant life.

“Economic deprivation could lead people to be lured into extremist groups.”

Kunyimwa uwezo wa kiuchumi: Hali ya kutokuwa na vitu vinavyokuwezesha kuishi maisha ya ustarabu.

“Kunyimwa uwezo wa kiuchumi hufanya watu wakavutiwa na vikundi vyenye misimamo mikali.”

Economic dynamics: Noun- /iː.kəˈnɒm.ɪk daɪˈnæm.ɪks/- Changes in an economic system over time, particularly those reflected in the behaviour of markets, businesses and the general economy.

“The economic dynamics have led to the wide gap between the rich and the poor.”

Mabadiliko ya kiuchumi: Mabadiliko yoyote yanayohusu masoko, biashara na uchumi kwa ujumla.

“Mabadiliko ya kiuchumi yamesababisha kuwepo kwa mwanya mkubwa baina ya matajiri na maskini.”

Economic pillar:- Noun- /iː.kəˈnɒm.ɪk pɪlə/- Strong supporter of an economy. In the context of CVE particularly County CVE Plans of Action, refers to the economic conditions that needs to be pursued and redistributed in society in order to prevent radicalization and extremism.

“Violent extremism affects tourism which is one of the economic pillars of the Kenyan economy.”

Mhimili wa kiuchumi: Kitu kinachochangia kuimarika kwa hali ya uchumi na kwa hivyo kuzuia uwezekano wa watu kujiingiza katika vitendo vya ghasia.
“Utalii ni mojawepo wa mihimili ya kiuchumi ya Kenya, kwa hivyo ukiimarisha utapunguza visa vya kigaidi.”

Economic prosperity: Noun- /i:.kə'nom.ɪk prɒs'per.ə.ti/- The state of being successful and having a lot of material things to the extent that you cannot be recruited to join extremist group for economic and or material gain.
“Economic prosperity of a person is a big factor in denouncing terror acts that may interfere with a conducive business environment.”

Ufanisi wa kiuchumi: Hali ya kushamiri na kuwa na fedha nyingi.
“Ufanisi wa kiuchumi wa nchi unategemea uwezewaji kiuchumi wa raia wote.”

Education: Noun- /edʒukeɪʃn/- A particular kind of teaching or learning.
“Those who get adequate education should shun extremist behaviours.”
Elimu: Njia ya kuongeza mafundisho, maarifa, masomo, tabia na uwezo wa watu.
“Watu wanaopata elimu katika jamii wanastahili kuwa kielelezo bora cha jinsi ya kuasi tabia za misimamo mikali.”

Education gap: Noun -/ 'edʒ.u.keɪʃn ɡæp/- It is the unequal distribution of those who are educated and those who are not educated.
“The education gap between the rich and the poor is widening.”

Mianya ya kielimu: Tofauti zilizoko baina ya waliosoma na wale wasiosoma.
“Mianya ya kielimu kati ya wale waliosoma na wasiosoma inaendelea kuwa mipana zaidi.”

Education transition: Noun- /edʒukeɪʃn trænziʃən/- The movement from one program to another in the education sector.
“There is low education transition in the marginalised communities of Kenya.”

Mpito wa kielimu: Hatua ya kutoka katika utaratibu mmoja hadi mwingine katika sekta ya elimu.
“Mpito wa kielimu ni wa kiwango cha chini sana miongoni mwa jamii zilizo-tengwa hapa Kenya.”

Eliminate: Verb- /i'ɪm.i.neɪt/ - To make someone or something not exist or to kill somebody especially an enemy or opponent.
“To eliminate someone is sacrilegious.”

Kuua: Kuondoa uhai wa mtu au kifanya mtu au kitu kukoma kuishi.
“Kuua mtu ni tendo la kinyama sana.”

Embrace: Verb- /ɪmˈbreɪs/- To accept an idea, a proposal or a set of beliefs.
“Many good citizens embrace peace.”

Kumbatia: Kukubali kitu bila maswali.

“Raia wengi wema hukumbatia amani.”

Emerging threats: Noun- /ɪˈmɜːdʒɪŋ θrets/- New, unforeseen and developing things or events that may cause harm or violence in society, especially if a particular action or order is not followed.

“The security agents must subvert all the emerging threats to peaceful co-existence.”

Vitisho Ibuka: Uwezekano wa kitu kibaya au ghasia kutokea hasa iwapo utaratibu fulani ama hatua fulani haikufuatwa.

“Lazima vyombo vya usalama vizime vitisho vyote ibuka ili watu waishi kwa amani.”

Enabling factors: Noun- /ɪˈneɪblɪŋ fæk.təs/- These are facts or situations that influence the result of something.

“The enabling factors that result into terror attacks are the availability of illegal arms and porous borders.”

Sababu zinazochangia: Hali au kitu kinachorahisisha utendekaji wa jambo fulani.

“Sababu zinazochangia mashambulizi ya kigaidi ni pamoja na upatikanaji wa silaha haramu na mipaka isiyolindwa vyema.”

Enforced disappearance: Noun- /ɪnˈfɔːst ˌdɪs.əˈpiːr.əns/- It is when a person is secretly abducted or imprisoned by a state or political organization or by a third party with the authorization, support, or acquiescence of a state or political organization, followed by a refusal to acknowledge the person's fate and whereabouts, with the intent of placing the victim outside the protection of the law.

“Instances of enforced disappearance are on the rise in the terror prone areas.”

Kupotea kulikopangwa: Hali ambayo mtu anatekwa nyara ama kufungwa kupitia kwa dola za serikali au vuguvugu la kisiasa na kisha kukana kuhusika au kujua alipo mtu huyo kwa nia ya kumzuia mtu huyo kulindwa na sheria zilizopo.

“Visa vya kupotea kulikopangwa vinazidi kuongezeka kila kukicha.”

Endemic poverty: Noun- /enˈdem.ɪk ˈpɒv.ə.ti/ This is an economic condition of life, regularly found and very common among a particular group or in a particular area.

“People who experience endemic poverty could be brainwashed to join terror groups.”

Umaskini wa kimaeneo: Hali ya kiuchumi inayotambulisha watu kutokana na janibu zao au kikundi chao.

“Watu wanaoishi katika umaskini wa kimaeneo wanaweza kupumbazwa kwa urahisi ili kujiunga na makundi ya kigaidi.”

Engagement: Noun -/In'geɪdʒ.mənt/- An arrangement to meet someone or do something at a particular time.

“The engagement of the youth in sensitization programmes should be encouraged.”

Miadi: Ahadi maalum inayowekwa ili itekelezwe kwa muda fulani au mahali fulani.

“Miadi miongoni mwa vijana katika taratibu za uhamasishaji inafaa kuhimizwa.”

Epitome: Noun- /i'pt.ə.mi/- The typical or highest example of a stated quality, as shown by a particular person or thing.

“To be a suicide bomber is the epitome of terrorism at individual level.”

Upeo: Kiwango cha juu zaidi cha ubora wa kitu kupitia kwa utendakazi wa mtu.

“Kuwa mlipuaji wa kujiuwa ni upeo wa ugaidi ambao mtu yeyote anaweza kufikia.”

Equality: Noun- /i'kwɒl.ə.ti/- The right of different groups of people to have a similar social position and receive the same treatment.

“Equality is a virtue which breeds fairness in all spheres of life.”

Usawa: Haki ya watu kuwa katika viwango vinavyofanana kiuchumi, kielimu na kisiasa.

“Usawa ni hulka inayoleta uwiano miongoni mwa raia.”

Erode: Verb- /i'rəʊd/- To slowly reduce or destroy something.

“Violence erodes the fabrics that unite a people together.”

Mong'onyoa: Punguza polepole au kuharibu kitu polepole.

“Ghasia humong'onyoa kila kitu kinachounganisha watu.”

Espionage: Noun- /'es.pi.ə.nɑ:ʒ/- The discovering of secrets, especially political or military information of another country or the industrial information of a business.

“The chancellor learned he was a victim of espionage when tiny cameras and microphones were found throughout his home.”

Kudoya: Kutambua siri, hasa za kisiasa au za kivita za nchi nyingine au kuvumbua siri za kibiashara za watu wengine.

“Aligundua kuwa yeye ni mhasiriwa wa kudoya baada ya kupata kamera ndogo ndogo na vinasa sauti kila mahali katika nyumba yake.”

Ethnic cleansing: Noun- /eθ.nɪk 'klen.zɪŋ/- The organized, often violent attempt by a particular cultural or racial group to completely remove, including by way of mass killings, from a country or area all members of a different ethnic, racial or political group or identity.

"Ethnic cleansing often leads to the killing of innocent people."

Mauaji ya kikabila: Jitihada zinazopangwa ili kushambulia kundi la kabila fulani ili kuliondoa kutoka kwa nchi au eneo fulani.

"Mauaji ya kikabila husababisha vifo vya watu wasiokuwa na hatia."

Ethnic relations: Noun- /'eθ.nɪk rɪ'leɪʃənz/- The relationships that exist between two people or communities that have different cultures and languages.

"Bad ethnic relations can lead to conflicts in a cosmopolitan region."

Mahusiano ya kikabila: Uhusiano uliopo baina ya watu ama jamii zilizo na tamaduni tofauti.

"Mahusiano mabaya ya kikabila huleta mizozo katika eneo lenye watu wenye utaiifa tofauti."

Evict: Verb- /ɪ'vɪkt/- To force someone to leave somewhere.

"No one should evict people from the pieces of land they have bought."

Kuhamisha: Kulazimisha mtu kutoka mahali amezoea kukaa.

"Hakuna anayeruhusiwa kumhamisha mwenzake kutoka kwa shamba alilounua."

Evolve: Verb- /ɪ'vɒlv/- To develop gradually, or to cause something or someone to develop gradually.

"Disaffection with governance styles can evolve into extremist responses."

Kuchipuka: Ni kukua polepole ama kusababisha kitu au mtu kuendelea polepole.

"Kutotosheka na uongozi wa serikali unaweza kuchipuka na kujigeuza katika misimamo mikali kupindukia."

Ex-combatants: Noun- /ɪks-kɒmbətənts/- Persons who were previously engaged in conflict.

"Ex-combatants should be taken to rehabilitation centres."

Aliyekuwa Mpiganaji: Mtu aliyeshiriki katika ghasia hasa zinazotokana na misimamo mikali.

"Aliyekuwa mpiganaji anayeongoka anafaa kupongezwa."

Execution: Noun- /,ek.sɪ'kjuː.ʃən/- It is killing someone in cold blood.

"The courts must guard against the execution of innocent citizens by security personnel under the guise of counter terrorism operations."

Adhabu ya kifo: Adhabu ya kifo inayotolewa kwa mtu asiyekuwa na hatia.

"Ni lazima mahakama zitahadhari dhidi ya kutoa adhabu ya kifo kwa watu wasiokuwa na hatia."

Exit: Verb- /'ek.st/ /'eg.zit/- It is the act of leaving something.

"To exit an extremist group could be a journey to positivism."

Toka: Kitendo cha kuacha kukaa mahali ama kuendelea kushiriki katika kitu fulani.

"Kutoka katika kikundi cha msimamo mkali si jambo rahisi lakini inaweze-kana."

Explicit risk analysis: Noun- /ɪk'splɪs.ɪt rɪsk/ /ə'næl.ə.sɪs/- This is clear and exact analysis of the possibilities of a bad thing happening.

"Prevention of crime can be effective with explicit risk analysis."

Uchanganuzi wazi wa hatari: Ni uchanganuzi wa kiparuwanja kuhusu uwezekano wa kutendeka kwa kitu kibaya.

"Inawezekana kuzuia uhalifu iwapo uchanganuzi wazi wa hatari utafanyika."

Extra-judicial killings: Noun- /'ek.strə.dʒu:'dɪʃ.əl 'kɪl.ɪŋs/- Unlawfull killings.

"Extra judicial killings should be condemned because they bring anger in the affected families."

Mauaji haramu: Mauaji yafanywayo bila ruhusa ya sheria na ambayo aghalabu hutekelezwa na vyombo vya dola.

"Mauaji haramu yanastahili kupingwa kwani huleta hasira miongoni mwa familia zilizoathirika."

Extremist: Noun- /ɪk'stri:.mɪst/- Someone who has beliefs that most people think are unreasonable and unacceptable.

"An extremist hardly sees things in others' way."

Mtu mwenye msimamo mkali: Mtu mwenye msimamo ambao haukumbatiwi na wengi wa watu katika jamii iliyostaarabika.

"Mtu mwenye msimamo mkali anafaa kupewa nasaha kwa upendo."

Extremism: Noun- /ɪk'stri:.mɪ.zəm/- The strong beliefs towards a doctrine or a teaching

"Extremism is a vice."

Msimamo mkali kupindukia: Hali ya mtu kuwa na mitazamo ambayo hai-kubaliki kwa walio wengi.

"Msimamo mkali kupindukia ni tishio kwa utangamano wa wananchi."

F

Facilitation: Noun- /fə.sɪl.ɪ'teɪ.jən/- To make something possible or easier.
"Facilitation of people to give intelligence information could help in identifying terror suspects."

Uwezeshaji: Kufanya kitu kifanyike kwa wepesi.
"Uwezeshaji wa watu kutoa habari za ushahidi dhidi ya maovu utasaidia kutambua washukiwa wa ugaidi."

Facilitation of a terrorist act: Phrase- /fə.sɪl.ɪ'teɪ.jən əv ə'ter.ə.rɪst ækt/- It is the act of helping other people to get into terrorist activities without getting directly involved in the process, discussion, etc. yourself.

"Facilitation of a terrorist act is majorly done by wealthy radicalised business people."

Udhamini wa vitendo vya kigaidi: Kusaidia watu kujiunga na vitendo vya kigaidi bila kujihusisha moja kwa moja.

"Udhamini wa vitendo vya kigaidi aghalabu hufanywa na mabwenyenye wenyewe dhana za kimageuzi."

Faith: Noun- /feɪθ/- It is great trust or confidence in something or someone.

"Everyone should have faith that the war on terror can be won."

Imani: Ni kuwa na tumaini katika kitu ama mtu.

"Kila mtu anafaa kuwa na imani kuwa tutashinda vita dhidi ya ugaidi."

Faith based ideologies: Noun- /'feɪθ.beɪst aɪ.di'ɒl.ə.dʒɪz/- These are a set of beliefs or principles, especially one on which religious organization are based.

"Faith based ideologies should be focused towards unity."

Fikira za kiimani: Fungu la kanuni za kidini zinazotawala shirika fulani.

"Fikira za kiimani zinastahili kuelekezwa katika juhudi za kuleta umoja."

False religious claims: Noun- /fɒls rɪ'lɪdʒ.əs kleɪm/- It is to say that something is true or is a fact, although you cannot prove it and other people might not believe it.

"Preachers who advance false religious claims should be barred from the houses of God."

Madai ya uongo ya kidini: Ni kusema mambo ambayo hayawezi kudhibitika kutoka kwa vitabu vya kidini ama kupinda ukweli wa kidini kwa nia mbaya.

"Wahubiri wanaoendeleza madai ya uongo ya kidini hawastahili kuruhusiwa kuingia katika maabadi."

Fighting:- /'fʌɪtɪŋ/- It is the act of displaying or engaging in violence, combat, or aggression.

"The fighting between Al-shabab and the Kenya Defence Forces claim a lot of lives."

Vita: Ni kitendo cha kupigana au kuhusika katika ghasia ama fujo.

Vita baina ya Al – Shabab na Majeshi ya Kenya vilisababisha vifo vingi.

Fighting skills: Noun- /'faɪ.tɪŋ skɪlz/- The abilities to do activities related to war, especially because you have practised them.

"The police must put up their best fighting skills against terror groups."

Stadi za kivita: Nyenzo na mbinu zinazohusiana na vita. Watu huzipata kwa kufanya mazoezi.

"Tunatoa mwito kwa polisi watumie stadi zao bora za kivita dhidi ya makundi ya kigaidi."

Foreign terrorist Fighters: Noun- /'fɔr.ən 'ter.ə.rɪst 'faɪ.təs/- They are individuals who travel to a State other than their State of residence or nationality for the purpose of the perpetration, planning or preparation of, or participation in, terrorist acts or the providing or receiving of terrorist training, including in connection with armed conflict.

"Foreign terrorist fighters are a big challenge to the local law enforcers."

Wapiganaji wa kigaidi kutoka nchi za kigeni: Ni watu wanaosafiri kwenda kwa taifa lililokuwa lao kwa kusudi la kupenyeza, kupanga ama kuhusika katika vitendo vya kigaidi kwa kutoa mafunzo na zana za kivita.

"Wapiganaji wa kigaidi kutoka nchi za kigeni ni tisho kubwa kwa vyombo vya usalama."

Financing: Noun- /fə'neɪn.sɪŋ/- To provide the money needed to do a particular thing, or the way of getting the money.

"Financing extremist activities is against the law."

Ufadhili wa kifedha: Kugharamia kifedha kitu au mtu.

"Kufadhili kifedha vitendo vinavyo vuruga amani ni kinyume cha sheria."

Flagship: Noun -/'flæɡ.ʃɪp/- The best or most important product, idea, building, etc. that an organization owns or produces.

"The flagship of intelligence chain has been launched."

Kuntu: Isiyo na ila; bora kabisa; kilichotukuka kwa sifa nzuri.

"Ukuntu wa utafutaji wa ushahidi umezinduliwa na serikali."

Forefront: Noun- /'fɔ:.frʌnt/- The most noticeable or important position.

"The president is in the forefront in the fight of violent extremism."

Mstari wa mbele: Kuwa katika nafasi muhimu na ya kuonekana.

"Rais yuko katika mstari wa mbele katika vita dhidi ya misimamo mikali inayo-endeleza ghasia."

Foreign bilateral partner: Noun- /'fɔː.ən baɪ'læt.ər.əl 'pɑːt.nər/- This is a partnership involving two parties.

"Uganda is Kenya's bilateral partner in the war of terrorism."

Mshirika mwenza: Ni ushirikiano unaohusisha pande mbili..

"Uganda ni mshirika mwenza wa kigeni kwa taifa la Kenya katika vita dhidi ya ugaidi."

Formative: Adjective- /'fɔː.mə.tɪv/- It is relating to the time when someone or something is starting to develop in character.

"Extremist activities should be nabbed at their formative stages."

Ulimbukeni: hali ya kufanya jambo kwa mara ya kwanza au ukosefu wa uzoefu.

"Vitendo vya watu wenye misimamo mikali vinafaa kukabiliwa wakati wa ulimbukeni."

Forums: Noun- /'fɔː.rəmz/- organised platforms in which people can talk about a problem or matter specially of public interest.

"Many forums that sensitize the youth against joining extremist groups should be encouraged."

Baraza: kongamano/mkusanyiko wa watu kujadili suala lililo na umuhimu wa umma.

"Tunafaa kuhimiza kongamano nyingi zaidi kuhusika katika uhamasishaji wa vijana dhidi ya ugaidi."

Freedom of religion: Phrase- /'friː.dəm ɒv rɪ 'lɪdʒ.ən/- The condition or right of being able or allowed to worship God or gods, or any such system of belief.

"Freedom of religion should not be misused for selfish gains."

Uhuru wa dini: Hali ya kuruhusiwa kisheria kuabudu Mungu ama miungu, ama chochote ambacho mtu anaamini ama haamini.

"Uhuru wa dini haufai kutumiwa vibaya kwa maslahi ya kibanafsi."

Freedom of expression: Phrase-/'friː.dəm ɒv ɪk'spreʃn/ - The right to express your opinions publicly.

"Freedom of expression should be accompanied by responsibility."

Uhuru wa kujieleza: Ni kuwa na haki ya kutoa hisia, mawazo ama maoni.

"Heri tuwajibikie uhuru wetu wa kujieleza."

Freedom of loving: Noun- /'friː.dəm ɒv 'lʌv.ɪŋ/- Self will to express or show affection.

"Kenyans have the freedom of loving their neighbours."

Uhuru wa Kupenda: mapenzi ya hiari kwa mtu mwingine.

"Wakenya wana uhuru wa kupenda majirani zao."

Fuelling conditions: Noun- /'fju:.əlɪŋ kən'dɪf•ənz/- All the particular things that influence or speed up something.

"Unwarranted arrests of suspects fueled conditions for the attacks."

Hali chochezi: Mambo ambayo hufanya kitu kifanyike kwa haraka zaidi.

"Kushikwa kwa watu wasiokuwa na hatia huleta hali chochezi ya mashambulizi ya ghasia."

Fundamentalist: /,fʌndə'mentəlɪst/- A person who believes in the strict, literal interpretation of scripture in a religion.

"People should interpret carefully the teachings of a religious fundamentalist."

Mwanamgambo: Mtu anayeamini katika itikadi kali ya kidini.

Watu wanafaa kutafsiri kwa makini mafundisho ya wanamgambo wa kidini.

Furtherance: Noun- /'fɜ:.ðərəs/- The process of helping something to develop or to be successful.

"Furtherance of false religious teachings should be condemned."

Endeleza: Hali ya kufanya kitu kifanikiwe.

"Uendelezwaji wa mafunzo ya uongo ya kidini ilaaniwe vikali."

G

Gangs: Noun- /gɑŋs/- An organised group of criminals.

"All gangs must be stopped before they expand their influence."

Genge: kundi la wahalifu.

"Lazima magenge yote yavunjwe ama yakabiliwe kabla ya kueneza uovu wao."

Generational clashes: Noun- /,dʒen.ə'reɪ.jənəl klæʃɪz/- these are disagreements or arguments between two people or groups of people who have different ages.

"Generational clashes can result into fights to inherit land."

Migongano ya kivizazi: Ni mabishano yanayotokana na mitazamo tofauti ya jinsi watu wanavyoona jambo kulingana na umri wao.

"Migongano ya kizazi inaweza kusababisha mapigano wakati wa maazimio ya kurithi shamba."

Genocidal activities: Noun- /ˌdʒen.əˈsaɪ.dəl ækˈtɪv.ə.tɪs/- These are acts that relate to the murder of a whole group of people, especially a whole nation, race, or religious group.

“Genocidal activities should be condemned by all nations.”

Mauaji ya kimbari: Mambo yoyote yanayohusu mipango ya kuangamiza kikundi cha watu kwa sababu ya kabila, imani au rangi yao.

“Tunafaa kulaani vitendo vyote vya mauaji ya kikabila.”

Global: Adjective- /ˈgləʊ.bəl/- relating to the whole world.

“The war on terrorism is a global agenda.”

Kiulimwengu: Inayohusu dunia nzima.

“Vita dhidi ya ugaidi vimekuwa mkondo wa ulimwengu.”

Global war on terror:- Noun: /ˈgləʊ.bəl wɔːr ɒn ˈter.ər/- This is the international engagement in the fight against terror activities.

“Global war on terror is taken seriously by all nations.”

Vita dhidi ya ugaidi ulimwenguni : Ni ushirikiano wa mataifa mbalimbali katika vita vya kupinga ugaidi.

“Vita dhidi ya ugaidi vitafaulu iwapo mataifa yote yatashirikiana.”

Governance: Noun- /ˈgʌvənəns/- The action or manner of governing a state or organisation.

“Good governance will ensure equity in distribution of resources.”

Utawala: Hali ya kuongoza taifa ama shirika.

“Utawala bora huhakikisha kuwa kuna usawazishaji katika mgao wa rasilimali.”

Gradual exposure: Noun- /ˈgrædʒ.u.əl ɪkˈspəʊ.ʒər/- The fact of experiencing something or being affected by it because of being in a particular situation or place over a long period of time.

“Gradual exposure to extremist teachings can brainwash the youth to believe in terror activities.”

Kujihusisha polepole: Kuwa katika hali ambapo hatari inatokea polepole.

“Mafundisho ya misimamo mikali kupindukia yanaweza kuhusisha vijana polepole na kisha kuwazuzua.”

Grappling: Verb- /ˈgræp.əlɪŋ/- To fight, work hard or persist, especially in order to win or get something.

“Many households are still grappling with poverty that has predisposed their sons and daughters to recruitment into extremist groups.”

Kukabiliana: Kupigana na kitu au hali ili kutwaa ushindi.

“Familia nyingi zinakabiliana na umaskini wa hali ya juu.”

Grievances: Noun- /gri:vənsɪs/- a real or imagined cause for complaint, especially unfair treatment.

"Peoples' grievances should be addressed amicably by the government."

Malalamishi: Maneno yanayosemwa na mtu au kundi la watu ili kuonyesha kutofurahishwa na jambo.

"Serikali inafaa kushughulikia malalamishi ya watu kwa njia ya kuridhisha."

Ground zero: Noun- /grəʊnd zɪərəʊ/- The beginning; starting point for an activity.

"The rehabilitation of the returnees should start at ground zero."

Shina: Asili au chimbuko la mtu au kitu fulani.

"Urekebishaji wa tabia kwa watu walioasi misimamo mikali kupindukia unastahili kuanzia mashinani."

H

Hard hit: Noun- /hɑ:d hɪt/- People who have been seriously affected by something.

"Mombasa and Mandera have been hard hit by terror groups."

Athirika zaidi: Hali ya kitu/sehemu/mtu kupata mapigo zaidi kutokana na kitu/jambo fulani.

"Mombasa na Mandera ni baadhi ya miji iliyoathirika zaidi kutokana na mashambulizi ya makundi ya kigaidi."

Haphazard investigations: Noun- /ˌhæpˈhæz.əd ɪnˌves.tɪˈgeɪ.jəns/- These are the processes of examining a crime, a problem that do not adhere to any obvious order or plan.

"Haphazard investigations can lead to conviction of innocent people."

Uchunguzi wa kiholelaholela: Mchakato wa kepeleleza visa vya uhalifu ambao hauzingatii utaratibu wowote maalum.

"Uchunguzi wa kiholelaholela huenda ukafanya watu wasiokuwa na hatia kutiwa mbaroni."

Harassment by security: Phrase- /ˈhær.əs.mənt baɪ sɪˈkjʊə.rə.ti/- These are the behaviours of the security agents that are annoying or upsetting to those affected.

"Harassment by security officers is against the law."

Kunyanyasa: Ni tabia za kuchukiza watu kutoka kwa maafisa walinda usalama.

"Dhuluma kutoka kwa maafisa wa usalama ni ukiukaji wa sheria za nchi."

Harm: Noun- /hɑ:m/- This could be physical or other injury or damage.
"It is unfair to harm innocent people."

Dhuru: Kuumiza kwa kujeruhi ama kuharibu.
"Sio haki kuwadhuru watu wasiokuwa na hatia."

Hero worshipping: Noun- /'hɪərəʊ ,wɜ:ʃɪpɪŋ/- A feeling of extreme admiration for someone, imagining that they have qualities or abilities that are better than anyone else's.

"Hero worshipping may lead the youth into extremist groups."

Kumsujudia mwanadamu: Toa heshima kubwa kwa mwanadamu ambayo mara nyingi inamfaa Muumba.

"Kumsujudia mwanadamu kunamkufuru Mungu."

Historical injustices: Noun- /hɪ'stɔrɪkəl ɪn'dʒʌs.tɪsɪz/- It is used to describe crimes or injustices that were committed in the past. In most cases, those historical crimes have formed the basis of grievances that push people to radicalization and extremism, that can be violent as well.

"Historical injustices must be addressed for the economically marginalised communities to feel that they belong to a country."

Dhuluma za kihistoria: Hutumika kuelezea uhalifu ama madhila ambayo watu hufanyiwa kwa miaka mingi.

"Baadhi ya jamii za pwani zinalalamikia maonevu ya kihistoria ambayo hulingana nao huendelezwa na serikali tofauti tofauti tangu uhuru."

Hopelessness: Adjective- /'həʊp.ləsni:s/- Inability or lack skill to effect a change or get what one desires making somebody to be discouraged.

"Many resort to join extremist groups because of hopelessness in life."

Tamauko: Kuondolewa tumaini la kupata kitu au kufanikiwa. Kukata tamaa.
"Watu wengi hukata shauri kujiunga na makundi yenye mirengo mikali kwa sababu ya tamauko maishani."

Hotspot: Noun- /'hɒt.spɒt/- A place where war or other fighting is likely to happen.

"Many hotspots of terror attacks are large business buildings and transport facilities."

Eneo hatari: Mahali ambapo pana uwezekano wa vita ama mapigano kufanyika.

"Maeneo mengi hatari ambayo mashambulizi ya kigaidi yanaweza kushuhudiwai ni majengo makubwa ya kibiashara na vyombo vya usafiri."

Humiliation: Noun- /hju:.mɪ.li'ei.jən/- To make someone feel ashamed or lose respect for himself or herself.

"Such kind of public humiliation should not be tolerated."

Dhalilisha: Kumfanya mtu atahayari ama akose heshima.

"Kumdhalilisha mtu mbele ya wengine sio kitu kizuri."

Human dignity: Noun- /'hju:.mən 'dɪg.nə.ti/- An individual or group's sense of self-respect and self-worth, physical and psychological integrity and empowerment.

"Everyone should uphold human dignity."

Hadhi ya mwanadamu: Heshima anayopata mtu hasa mbele ya watu wengine.

"Kila mtu anafaa kudumisha hadhi ya kimwanadamu."

Human rights: Noun- /'hju:.mən 'raɪts/- The basic rights that it is generally considered all people should have or enjoy, such as justice and the freedom of expression, association and belonging.

"The government should encourage the upholding of the citizens' human rights."

Haki za kibinadamu: Vitu au mambo ambayo ni stahiki ya mtu kama vile kupata elimu.

"Serikali inahitajika kutilia mkazo haki zote za kibinadamu."



Idle youths:- Noun- /'aɪ.dəl ju:θs/- Not employed youths; youths unoccupied with business; inactive youths; doing nothing.

"Idle youths are prone to drug abuse and radicalisation."

Vijana wasiokuwa na shughuli maalum: Vijana wasiokuwa na kazi wala biashara.

"Ni rahisi kuwavuta vijana wasiokuwa na ajira katika itikadi kali na matumizi ya mihadarati."

Identity:- Noun- /aɪ den.tɪ./- The state or quality of being the same; sameness, belonging or sharing a particular trait or practice.

“The identity of the fingerprints on the gun with those on file provided evidence that he was the killer.”

Tambulishi: Hali ya kufanana au kuwa na sifa zinazofanana kama vile watu kuwa na sifa za kigaidi.

“Tambulishi za vidole kwenye bunduki zilikuwa ushahidi fika kuwa yeye alikuwa muuaji.”

Ideologies:- Noun- /ˌaɪ.dɪ.əˈdʒi.zɪs/- An orientation that characterizes the thinking of a group or nation.

“Religious ideologies are sources of radicalization in the world.”

Dhana: Wazo ama fikra inayojengeka kichwani mwa mtu.

“Baadhi ya dhana za kidini zinapotosha vijana.”

Ideological construct:- Noun- /ˌaɪ.di.əˈlɒdʒ.i.kəl kənˈstrʌkt/- To put or build ideas or put together different views to form something whole.

“Solutions will come from positive ideological construct.”

Ujenzi wa kidhana: Kuweka mawazo au imani pamoja ili kusababisha mtazamo fulani.

“Suluhu zitapatikana iwapo kutakuwa na ujenzi chanya wa kidhana.”

Ignorance:- Noun- /ˈɪɡnərəns/- The lack of knowledge in general, or in relation to a particular subject; the state of being uneducated or uninformed.

“Many young people have joined extremist groups because of their ignorance of religious teachings and philosophy.”

Kutojua: Ukosefu wa maarifa kuhusu suala fulani.

“Watu wasitumie kutojua kama kisingizio cha kujiingiza katika makundi haramu.”

Immunity: Noun - /ɪˈmjuːnəti/- Freedom or exemption from any charge, duty, obligation, imposition, penalty, or service; a particular privilege.

“Juma was given immunity by the government for disclosing confidential information.”

Kutopasiwa: kinga ya kutochukuliwa hatua kama vile kushtakiwa, na kadhalika.

“Juma alipewa kinga ya kutochukuliwa atua na serikali kwa ajili ya kutoa habari za siri.”

Impact:- Noun- /ˈɪm.pækt/- A powerful effect that something, especially something new, has on a situation or person.

“Terror activities are having a major impact on our economy.”

Athari: Matokeo yanayoachwa kutokana na tukio Fulani hasa kutokana na kitu kigeni kwa hali au mtu.

"Vitendo vya kigaidi huacha athari kubwa kwa uchumi wetu."

Implicate:- Verb- /'ɪm.plɪ.keɪt/- To show that someone is involved in a crime or partly responsible for something bad that has happened.

"The women were implicated in the Mombasa central police station attacks."

Kumpata mtu na Makosa: Kuudhihirisha kuwa mtu fulani alihusika kwa njia moja ama nyingine katika tendo la kihalifu.

"Wanawake walipatika na makosa ya mashambulizi ya Kituo cha Polisi cha Mombasa."

Improvised Explosive Devices: /ɪm.pri.vəɪzd ɪk.spləʊsɪv dɪ.vaɪsɪs/- It is a bomb constructed and deployed in ways other than in conventional military action.

"Improvised Explosive Devices (IED) were used extensively in the Garrissa and West gate mall attacks."

Vilipuzi vya kujitengenezea: Vifaa mfano wa bomu ambavyo ni vya kujitengenezea.

"Vilipuzi vya kujitengenezea vilitumiwa katika mashambulizi ya Chuo Kikuu cha Garissa na Duka la West Gate."

Incitement to terrorism: Phrase- /ɪn'saɪt.mənt tu: 'ter.ər.ɪ.zəm/- It is to influence someone to do or be part of terror activities.

"Incitement to terrorism is punishable by law."

Uchochezi wa kigaidi: Ni kuhimiza mtu kushiriki katika vitendo vya kigaidi.

"Uchochezi wa kigaidi ni kosa mbele ya sheria."

Indigenous communities:- Noun- /ɪn'dɪdʒ.ɪ.nəs kə'mju:.nə.tɪz/- They are inhabitants and practitioners of unique cultures and ways of relating to people and the environment.

"Historical injustices, including traditional land claims, have made indigenous communities in the coast such as Mijikenda, to be vulnerable to extremist narratives that hype fairness and economic redistribution once they topple secular governments."

Jamii za kiasili: Wenyenji wa mazingira fulani.

"Hujuma za kihistoria, ikiwa pamoja na ukosefu wa haki za mashamba, zimefanya jamii za kiasili za pwani kama vile Wamijikenda, kuwa rahisi kupenyezwa na misimamo mikali kupindukia ambayo huahidi ugavi wa rasilimali za kiuchumi pindi serikali dhalimu inapopinduliwa."

Ineffective: Adjective - /,ɪn.ɪ'fek.tɪv/- Not producing an intended effect;
"An ineffective teacher cannot handle issues on violent extremism."

Kutotenda vilivyo: Kukosa uwezo wa kutekeleza kama itakikanavyo.
"Walimu wasiokuwa na uwezo kutenda vilivyo hawawezi kushughulikia masuala ya misimamo mikali."

Inefficient: Adjective - /,ɪn.ɪ'fɪ.ənt/- Lacking the ability or skill to perform effectively; inadequate.

"Inefficient communities cannot curb terror attacks."

Uhaba wa maarifa: Hali ya mtu kukosa uwezo ama ustadi wa kufanya kazi vizuri.

"Jamii zinazo kuwa na uhaba wa maarifa haziwezi kuzuia mashambulizi ya kigaidi."

Initiatives:- Noun- /ɪ'nɪʃ.ə.tɪvz/- A plan or process to achieve something or solve a problem.

"The locals must take the initiative to end violent extremism."

Mikakati: Mipango inayoandaliwa kwa makini kabisa kwa lengo la kutekeleza jambo fulani."

"Ni muhimu wenyeji wafanye mikakati ya kumaliza misimamo mikali ya ghasia."

Integrate: Verb- /'ɪn.tɪ.greɪt/- Make into a whole or make part of a whole or to bring back into the society.

"County CVE Forums seek to integrate every stakeholder in the county into the CVE agenda."

Fungamanisha: Jumuisha au shirikisha katika ngazi mbalimbali za maisha.
"Alifungamanishwa katika jamii baada ya kuachana na vitendo vya kihalifu."

Intelligence: Noun - /ɪn'tel.ɪ.dʒəns/- The ability to secretly gather and interpret information about a group or certain issues.

"The police gathered enough intelligence before arresting the terror suspect."

Ujasusi: Utafutaji wa habari za kisiri.

"Kitengo cha ujasusi kimekuwa kikifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na mataifa jirani ili kupata habari muhimu."

Intercept: Verb - /ɪntə'sept/- To obstruct or interrupt the progress of; to stop; to hinder or oppose.

"The community should not intercept the arrest by police of terror suspect"

Zuia: Kumkataza mtu kufanya jambo kwa kumuogofya ama kupunguza ari ya mtu ya kufanya kitu fulani.

"Misafara ya watu waliojiunga na makundi ya kigaidi inafaa kuzuiwa."

Interfaith dialogues: Noun- /ɪn.tə'feɪθ'daɪ.ə.lɒɡs/- Cooperative, constructive, and positive interaction between people of different religious traditions (i.e., "faiths") and/or spiritual or humanistic beliefs, at both the individual and institutional levels.

"Issues of violent extremism require intervention of various inter faith dialogues to curb the issue."

Midahalo ya kidini: Mazungumzo miongoni mwa watu wa imani mbalimbali
"Masuala yanayohusu misimamo mikali ya vurugu yanahitaji kuingiliwa kati na midahalo ya kidini."

Interlocutors: Noun- /ɪn.tə'lɒk.jə.təs/- People who take part in dialogue or conversation; talkers, interpreters, or questioners.

"She played a key role as the interlocutor in the debate about gender and extremism."

Wajumbe: Wale wanaoshiriki katika mdahalo; katika kuzungumza, kutafsiri, ama kuuliza maswali.

"Wajumbe kutoka mataifa mbalimbali watajumuika katika mji wa Mombasa ili kuzungumzia suala nyeti la misimamo mikali kupindukia ya ghasia."

Intermediary: Noun- /ɪntəmi:dɪəri/- One who takes part in dialogue or conversation; a talker, interpreter, or questioner.

"He was the intermediary between the two conflicting communities."

Mpatanishi: Yule anayeshiriki katika unganishaji wa suluhu baina ya watu ama makundi ya watu wanaozozana.

"Alikuwa mpatanishi baina ya jamii mbili zilizokuwa zikizozana."

Intervening efforts: Noun- /ɪn.tə'vi:.nɪŋ'ef.ət/- It is trying to come between disputing people, groups, etc.; intercede; mediate.

"All the intervening efforts must be tried to stop terrorism."

Jitihada za kuingilia kati: Ni kujaribu kusuluhisha tofauti kati ya makundi ya watu.

"Ni muhimu jitihada zote za kuingilia kati zitumike ili kuzuia ugaidi."

Interventions:- Noun- /ɪn.tər'ven'ʃəns/- The act or fact of being involved intentionally in a difficult situation.

"The interventions of the locals saved his life."

Kuingilia kati: Kufanya juhudi za kimakusudi katika upatikanaji wa suluhu katika hali fulani ngumu.

"Juhudi za watu wake za kuingilia kati ziliokoa maisha yake."

Interventionist activities: Noun- /ɪn.tə'ven.ʃən.ɪst æk'tɪv.ə.tɪz/ - These are the actions or plans that a government put in place in order to be involved in sorting out a problem in a country or in another country.

"The interventionist activities initiated by the government are the best to counter violent extremism in Kenya and Somalia."

Vitendo vya kuingilia kati: Mikakati inayowekwa kusuluhisha matukio Fulani.

“Vitendo vya kuingilia kati kutoka kwa serikali vitafaa sana katika hali hii ya kupambana na suala la ugaidi”

Intimidation: Noun- /ɪntɪmɪdeɪʃn/ - It is to forcefully compel, frighten or threaten someone to do something he/she doesn't want.

“Families affected by terrorism alleged all manners of harassment and intimidation from security agents.”

Vitisho: Hali ya kutia mtu hofu na kumfanya mnyonge.

“Mara nyingi watu husukumwa kwa vitisho ili kujisajili na vikundi haramu vya ugaidi.”

Intolerance: Noun - /ɪntələrəns/- Unwillingness to recognize and respect differences in opinions or beliefs.

“Intolerance of other religions and or political ideologies are often the seeds of radicalization and violent extremism in a society.”

Kutovumiliana: Watu kukosa uwezo wa kutambua na kuheshimu mawazo na maoni ya wengine, kutokuwa na subra.

“Misimamo mikali kupindukia hutokea kwa sababu ya watu wenye mitazamo pinzani kukosa kuvumiliana.”

Intrusive: Adjective- /ɪntruːsɪv/- Tending or opt to intrude; coming without invitation or consent.

“Intrusive reporting can cause chaos in war torn communities.”

Dukiza: Enda mahali ama kujihusisha katika jambo bila kualikwa.

“Tabia ya kudukiza inaweza kuleta hali ya sintofahamu miongoni mwa watu.”

J

Investigation: Noun- /ɪnvestɪgeɪʃn/- A searching inquiry for ascertaining facts; detailed or careful examination.

“Was there an investigation on the terror suspects before they were prosecuted?”

Uchunguzi: Hali ya kupekua ama kutafuta ukweli kuhusu kitu.

“Je, washukiwa wa ugaidi walifanyiwa uchunguzi wowote kabla ya kushitakiwa?”

Muslim: Noun- /muzlɪm, 'muslɪm, 'mʌzlɪm /- A believer or follower of Islam.

“The Coastal region has a higher number of Muslims compared to Christians.”

Uislamu: Muumini wa dini ya kiislamu.

“Waislamu ni wengi kuliko Wakristo katika ukanda wa Pwani.”

Islam: Noun- /ɪzləm/- The act of believing in islamic norms which govern their civilization and way of life.

“Islam as a religion stands and advocates for peace contrary to the misinterpretation that Islam abets violence in the name of Jihad.”

Uislamu: Dini inayosimamia nguzo za Korani Tukufu.

“Uislamu ni dini iliyojengeka kwenye mihimili ya amani.”

Jihad: Noun- /dʒə'hæd/- A holy war waged on behalf of Islam as a religious duty; also: a personal struggle in devotion to Islam especially involving spiritual discipline.

“The spiritual leader declared Jihad against the infidels.”

Jihadi: Vita vitakatifu vinavyopiganwa kwa niaba ya Uislamu kama jukumu la kidini: Aidha, ni jukumu la kibanafsi linaloonyesha kujitoa mhanga kama ishara ya nidhamu ya kidini.

“Kiongozi wa kidini alitangaza vita vya jihadi dhidi ya makafiri.”

Jihadist: Noun- /dʒə'hædist/- A Muslim who is involved in a jihad.

“All the Jihadists prayed at dawn.”

Mwanajihadi: Muislamu anayejihusisha katika vita vya jihadi.

“Wanajihadi wote waliswali wakati wa mapambazuko.”

Joint effort: Noun: /dʒɔɪnt efət/- Something that is done by two or more people or groups working together.

“Fighting violent extremism should be a joint effort of all stakeholders.”

Jitihada za pamoja: hali ya ushirikiano katika kufanya jambo.

“Tunahitaji jitihada za pamoja kati ya serikali, viongozi wa kidini na mashirika ya kibinafsi ili kushinda vita dhidi ya misimamo mikali kupindukia.”

Judgement: Noun- /'dʒʌdʒmənt/- The ability to comprehend, make a decision, or form an opinion objectively, authoritatively, and wisely, especially in matters affecting action.

“But it's one thing to judge victims of violent extremism, and another to impose your judgement coercively.”

Hukumu: Kuwa na uwezo wa kuelewa, kufanya uamuzi au kuwa na maoni kuhusu suala fulani bila mapendeleo, kwa hekima hususan katika masuala yanayotakikana uchukuaji wa hatua.

“Si jambo la busara kuhukumu washukiwa wa msimamo mkali wa fujo bila kuwapa nafasi ya kusikilizwa.”



Justice: Noun- /dʒʌstɪs/- The quality of being fair; righteousness, equitableness, or moral rightness.

“All Kenyans should be treated equally and justice should apply to all despite colour, race and tribe.”

Haki: Uwezo wa kuwa mtu asiyekuwa na mapendeleo, mwenye haki na mwadilifu.

“Wakenya wote wanafaa kupewa usawa na haki itendeke kwa kila mtu pasi kujali rangi, dini wala kabila.”

Land alienation: Noun- /lænd ˌeɪ.li.əˈneɪ.jən/- the feeling that you have no connection or ownership of land.

“Land alienation has made many people to become hopeless.”

Utengaji wa ardhi: Mtu kuhisi kuwa hana uhusiano wala uwezo wa kumiliki shamba.

“Utengaji wa ardhi huwafanya watu kukosa tumaini na kwa hivyo kushawishika kwa urahisi kujiunga na vikundi haramu vya kihalifu.”

Law abiding: /lɔː əˈbaɪ.dɪŋ/- (Of individuals) adhering strictly to laws and rules and customs;

“The law-abiding citizens have nothing to fear from government surveillance.”

Kutii sheria: Kufuata kanuni na tamaduni fulani.

“raia wanaotii sheria hawana hofu kwa uchunguzi wa serikali.”

Law enforcement: /lɔː ɪnˈfɔːsmənt/- It is ensuring obedience to law.

